

**P R E P**  
**V A C C**



## **Jiunge na utafiti mmoja. Pima njia mbili za kuzuia VVU. Kwa wakati mmoja.**

Mradi wa kuzuia maambukizi ya VVU inayotathmini chanjo za majaribio ya VVU na dawa kinga ya VVU ya kumeza (PrEP) unaoongozwa na watafiti wa Afrika, wakisaidiana na watafiti wa Ulaya.



### **Utafiti huu wa PrEPVacc ni nini?**

PrEPVacc ni vitu viwili:

Ni kupima kama aina mbili za mchanganyiko wa chanjo ya majaribio zinaweza kuingia dhidi ya VVU. Aina zote hizi mbili za mchanganyiko tayari zilishajaribiwa kwenye tafiti za kitabibu na zimeonyesha usalama wake

Na kwa wakati huo huo, inapima aina mpya ya dawa kinga ya VVU (PrEP) dhidi ya dawa kinga ya VVU (PrEP) inayotumika sasa.

### **Utafiti uko wapi?**

Utafiti huu unapangwa kufanyika kwenye vituo vitano katika nchi 4: Masaka, Uganda; Mbeya, Tanzania; Dar-es-Salaam, Tanzania; Maputo, Msumbiji na Durban, Afrika Kusini.

### **Chanjo ya VVU ni nini?**

Chanjo inafundisha mwili kujikinga dhidi ya maambukizi fulani au kupigana na ugonjwa kwaajili ya kukuweka na afya njema. Dunia bado haina chanjo inayo kinga VVU iliyosajiliwa. Ili kutengeneza chanjo, watafiti wanahitaji kuipima kwa watu, ili kugundua kama itaweza kusaidia kuingia au kupigana na VVU. Inatolewa kwa sindano.

### **Dawa Kinga ya VVU ya Kumeza (Oral PrEP) ni nini?**

Dawa Kinga ya VVU (PrEP) ni matumizi ya dawa za kufubaza VVU kwa watu wasio na maambukizi ya VVU ili kupunguza hatari yao ya kupata maambukizi ya VVU. Dawa Kinga ya VVU imeonyesha kuzuia VVU na inapatikana duniani kama kidonge.

### **Utatoa mchango gani kwa kushiriki?**

Kuna njia nyingi za kuzuia VVU, ila kila mwaka maambukizi mapya yanaendelea kuripotiwa. Ushiriki wako na jitihada zako zitasaidia kujibu maswali mawili kwa taarifa ambazo zinaweza kusaidia kuzuia maambukizi mapya kwenye jamii yako.

- Tutaweza kusema iwapo utengenezwaji wa aidha ya mchanganyiko miwili ya chanjo ya kuzuia VVU inafaa au la
- Tutaweza kusema kama aina mpya ya dawa kinga ya VVU (PrEP) inakubalika, ni salama na ina ufanisi kama aina ya dawa kinga ya VVU ya kumeza inayotumika kwa hivi sasa na wanawake pamoja na wanaume

Wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 18–40 wenye hatari ya kupata maambukizi ya VVU wanaalikwa kushiriki kwenye utafiti wa PrEPVacc.

### Unaweza kushiriki kama:

- Unaafya njema
- Una umri wa miaka 18–40 siku ya mchujo
- Unautayari na unauwezo wa kutoa ridhaa kushiriki kwenye utafiti huu
- Unautayari na unaweza kuja katika mahudhuri yote na kufanyiwa kipimo cha VVU na kutoa damu, mkojo na sampuli zingine kwa wakati zinapohitajika

### Afya na haki za washiriki zitalindwa vipi?

Wakati wote tutawapa washiriki taarifa kamili kuhusu utafiti kabla mshiriki hajajiunga kwenye utafiti, ili uweze kutupa ridhaa ya kushiriki.

Washiriki wana haki ya kujitoa kwenye utafiti wakati wowote.

Kipindi cha utafiti, wafanyakazi wa kliniki watawafuatilia washiriki ili kuhakikisha kwamba chanjo na dawa kinga dhidi ya VVU hazisababishi matatizo yoyote ya kiafya.

Wafanyakazi wa utafiti pia, watawasaidia washiriki kuripoti matatizo yoyote ya kijamii ambayo wanapata kutokana na kuwepo kwenye utafiti.

Usalama wa washiriki upo chini ya uangalizi wa timu inayofuatilia usalama na bodi ya kujitegemea ya ufuatiliaji wa usalama ambayo mara kwa mara huangalia taarifa za kiafya za washiriki na kuamua kama ni salama kuendelea na chanjo na dawa kinga ya VVU.

Kamati ya maadili ya kitaasisi inapitia na kufuatilia mpango wa utafiti kwa kila kituo kinachofanya utafiti huu, pamoja na taarifa inayotolewa kwa watu kuhusu utafiti huu, maendeleo ya utafiti, na matatizo ya kiafya ya washiriki. Kamati hii ya maadili pia huangalia kama haki za washiriki zinaheshimiwa.

Kila kliniki ya utafiti ina bodi ya ushauri wa jamii. Wajumbe wake ni watu wa mahali hapo hapo ambao wanashauri watafiti na kuleta wasiwasi na masilahi ya jamii na washiriki wa utafiti kwa watafiti.



### Vipi kama sitaki kushiriki?

Ushiriki wako ni hiari kabisa, na ni juu yako wewe kuamua aidha kushiriki au la. Endapo utaamua kushiriki, unaweza kujitoa wakati wowote bila kutoa sababu. Hii haitaathiri huduma unayopata kutoka kliniki kwa namna yoyote.



### **Ni athari gani zitarajiwazo?**

Kama ilivyo kwa dawa na chanjo nyingi tunazotumia, tunafahamu kuwa kuna uwezekano wa kupata athari ndogo ndogo. Athari hizi zinaweza kuwa homa, kichwa kuuma, kichefuchefu, maumivu na uchovu.

Kwa baadhi ya watu, dawa kinga ya VVU inaweza kusababisha athari ndogo ndogo kama kichefuchefu, hisia ya tumbo kujaa, kuharisha na kuumwa kichwa. Madhara haya madogo madogo hupotea kadri muda unavyoenda.

### **Nitakingwa dhidi ya VVU endapo nikijiunga na utafiti?**

Bado hatufahamu kama chanjo za utafiti huu zitakinga washiriki dhidi ya VVU. Watu wanaotumia dawa kinga ya VVU (PrEP) vizuri, hawana uwezekano mkubwa wa kupata VVU.

Washiriki wote watapewa ushauri nasaha ya jinsi ya kuzuia maambukizi ya VVU na watahimizwa kutumia njia za kuzuia zilizopo kupitia utafiti huu.

### **Itachukua muda gani kujua kama bidhaa za utafiti zinafanya kazi?**

Tunatarajia utafiti utakamilika mwezi wa tatu 2023 na kujifunza kama chanjo za utafiti na dawa kinga mpya ya VVU (PrEP) zinakinga maambukizi ya VVU kwa kipindi hicho, ila inawezekana kufahamu mapema.

Washiriki na watafiti watapatiwa taarifa hizi zitakapopatikana.

### **Je, kushiriki kwenye utafiti huu kutaathiri maisha yangu binafsi kwa namna fulani?**

Tunawaomba wanawake kutumia njia za kuzuia mimba ili wasipate ujauzito katika kipindi cha utafiti, (kutoka mchujio wa awali hadi baada ya wiki 18 baada ya chanjo ya mwisho kwasababu hatujui athari za chanjo hii kwa mtoto anaekua. Tunawaomba wanaume wajizuie kusababisha wenzi wao wa kike ujauzito kwenye kipindi cha utafiti hadi wiki 18 baada ya chanjo ya mwisho kwa sababu hiyo hiyo.

### **Chanjo zinaweza kukupa VVU?**

Hapana. HAIWEZEKANI KABISA kupata maambukizi ya VVU kutokana na chanjo zinazotumika kwenye utafiti huu. Chanjo hazina kirusi cha VVU kilichohai, kirusi cha VVU kilichouwawa, sehemu zilizochukuliwa kutoka kwenye kirusi cha VVU au seli zilizoathirika na VVU. Chanjo zimetengenezwa na sehemu za kemikali salama.

### **Nitatakiwa kufanya nini endapo nitashiriki?**

Ushiriki wako katika utafiti wa PrEPVacc utadumu kwa angalau miezi 17 kutoka sindano ya kwanza ya chanjo. Kutakuwa na angalau mahudhurio 15 wakati wa utafiti. Mahudhurio yatajumuisha taratibu mbalimbali, ushauri nasaha, kujifunza kutokana na uzoefu wako, kupata taarifa kuhusu afya yako kwa wakati husika, kujibu maswali kuhusu matendo na tabia yako ya kujamiiiana, pamoja na kuchukua damu na sampuli za mkojo. Yatadumu kwa hususani saa 1–3 kila moja.

Utapewa mchanganuo wa kina wa nini kinachotokea katika kila hudhurio ili ujue nini cha kutarajia. Utafidiwa gharama zako za nauli za kwenda kliniki.

### **Chanjo**

Mchanganyiko mmoja unachanganya vinasaba (DNA) na chanjo yenye protini, na mwingine unachanganya vinasaba (DNA), MVA na chanjo yenye protini. Baadhi ya washiriki watapata vipozaungo ambayo haina chanjo, ambayo itakuwa ni vimiminika safi na salama inayoitwa chumvi.

### **Dawa Kinga (PrEP)**

PrEPVacc itajaribu kama aina mpya ya dawa kinga ya VVU (PrEP) ya kumeza, TAF/FTC (Descovy) yakumeza kila siku, ina ufanisi sawa au zaidi kuliko TDF/FTC (Truvada) yakumeza kila siku. Washiriki watapewa dawa kinga ya VVU (PrEP) kipindi cha awamu ya chanjo (miezi 6) ili kukinga VVU.

## Nani anaendesha PrEPVacc?

PrEPVacc inaongozwa na watafiti wa Kiafrika kutoka Entebbe, Uganda, katika Baraza la Utafiti la Utabibu (MRC)/Taasisi ya utafiti wa Virusi cha Uganda (UVRI) na Chuo cha afya na magonjwa ya tropiki cha London (LSHTM) kituo cha utafiti Uganda. Wakisaidiana na washirika 14, sita kutoka Afrika, sita kutoka Ulaya na wawili kutoka Marekani. Mfadhili wa PrEPVacc ni Chuo cha Imperial London.

## Nifanye nini baada ya hapa?

Endapo baada ya kusoma kipeperushi hiki, una maswali au nia ya kushiriki kwenye utafiti wa PrEPVacc, tafadhali wasiliana na kituo kama ifuatavyo;



*Watafiti wa PrEPVacc wa Dar es Salaam.*



*Watafiti wa PrEPVacc wa Mbeya.*

<b>Dar-es-Salaam, Tanzania</b>	<b>Prof. Said About</b> (Mtafiti Mkuu) <b>Dr. Patricia Munseri</b> (Mratibu wa Utafiti) <b>Ms Mary Ngatoluwa</b> (Muuguzi Mkuu wa Utafiti)	<b>0754 301 692</b> <b>0744 562 784</b> <b>0784 608 842</b>
<b>Mbeya, Tanzania</b>	<b>Dr Wiston William</b> (Mtafiti Mkuu wa Utafiti) <b>Dr Emmanuel Kapesa</b> (Mratibu wa Utafiti)	<b>+255 768685076</b> <b>+255 766859916</b>



Mradi huu ni sehemu ya programu ya pili ya Ushirikiano katika Tafiti za Kitabibu kati ya Nchi za Ulaya na Nchi Zilizozendelea (EDCTP2) unaosaidiwa na umoja wa ulaya. © Watafiti wa PrEPVacc 2019

### Photography

PrEPVacc Investigators /  
Frank and Helena Herhold